
# MWELEKEO WA MVUA ZA MSIMU WA VULI (OKTOBA – DESEMBA), 2026




***Kielelezo 1: Mwelekeo wa mvua za Vuli (Oktoba hadi Desemba), 2026.***


*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz



**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

## Dondoo muhimu za msimu wa mvua za Vuli (Oktoba – Desemba), 2026

Taarifa hii inatoa uchambuzi wa mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na kutoa mwelekeo wa msimu wa mvua za Vuli (Oktoba hadi Desemba), 2026. Pia, inawasilisha ushauri na tahadhari za mapema kwa wadau wa sekta mbalimbali ambazo zimekuwa zikiathiriwa na mabadiliko ya hali ya hewa kama vile Kilimo na Usalama wa chakula, Mifugo na Uvuvi, Utalii na Wanyamapori, Usafiri na Usafirishaji (nchi kavu, kwenye maji na angani), Mamlaka za Miji, Sekta Binafsi, Vyombo vya Habari, Nishati, Ujenzi, Maji na Madini, Afya pamoja na Menejimenti za Maafa. Utabiri huu ni mahsusi kwa maeneo (Nyanda za juu kaskazini mashariki, Pwani ya kaskazini, Ukanda wa Ziwa Viktoria pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma) yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Kwa muhtasari, mwelekeo huo na athari zake unaonesha kuwa**:**

### a) Mvua za msimu wa Vuli, 2026

i. Msimu wa mvua za Vuli, 2026 unatarajiwa kuathiriwa kwa kiwango kikubwa na hali ya El Niño yenye nguvu kubwa.

ii. Mvua za Vuli, 2026 zinatarajiwa kuwa za Juu ya Wastani hadi Wastani katika maeneo mengi ya Ukanda wa Pwani ya Kaskazini, Nyanda za Juu Kaskazini Mashariki, Ukanda wa Ziwa Viktoria na kaskazini mwa Mkoa wa Kigoma.

iii. Mvua za Vuli, 2026 zinatarajiwa kuanza wiki ya nne ya mwezi Septemba na wiki ya kwanza ya mwezi Oktoba, 2026 katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Viktoria na baadae kusambaa taratibu katika maeneo mengine mwezi Oktoba. Kwa kawaida, mvua za Vuli huisha mwezi Desemba; hata hivyo, katika msimu huu mvua za nje ya msimu zinatarajiwa kuendelea hadi mwezi Januari, 2027.

iv. Ongezeko la mvua linatarajiwa katika kipindi cha mwezi Novemba, 2026.

### b) Athari zinazotarajiwa

i. Vipindi vya unyevu kwenye udongo wa kuzidi kiasi pamoja na mafuriko vinaweza kujitokeza na kuathiri ukuaji wa mazao na miundombinu ya kilimo. Hata hivyo, katika baadhi ya maeneo shughuli za kilimo zinatarajiwa kuendelea kama kawaida katika msimu huu wa Vuli, 2026.

ii. Ongezeko la kina cha maji katika mabwawa na mito linatarajiwa kujitokeza, hali ambayo inaweza kuathiri miundombinu ya rasilimali za maji na nishati.

iii. Magonjwa ya mlipuko yanaweza kujitokeza kutokana na uchafuzi wa maji.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

## 1. MWELEKEO WA MVUA ZA VULI (OKTOBA – DESEMBA), 2026

Msimu wa mvua za Vuli ni mahususi kwa maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), pwani ya kaskazini (kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, mikoa ya Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia), Dar es Salaam, Tanga pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba), ukanda wa Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu na Mara) pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma.

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa inayotarajiwa katika kipindi cha Vuli (kama inavyoelezwa katika kipengele cha 2 cha taarifa hii), kwa ujumla mvua za Juu ya Wastani hadi Wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Mara, Arusha, Manyara, Kilimanjaro, kaskazini mwa mkoa wa Kigoma, Dar es Salaam, Tanga, Pwani (ikiwemo visiwa vya Mafia), kaskazini mwa mkoa wa Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba. Kwa kawaida mvua za Vuli huisha mwezi Desemba, hata hivyo msimu huu mvua za nje ya msimu zinatarajiwa kuendelea hadi mwezi Januari, 2027. Ongezeko la mvua linatarajiwa mwezi Novemba, 2026.

Maelezo ya kina juu ya mwelekeo wa mvua hizo za msimu ni kama ifuatavyo:

### i. Kanda ya Ziwa Victoria: (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, na Mara) pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma (wilaya za Kakonko na Kibondo):

Mvua za Vuli zinatarajiwa kuwa za Juu ya Wastani hadi Wastani katika maeneo ya mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Mara pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma.

Mvua hizo zinatarajiwa kuanza wiki ya nne ya mwezi Septemba hadi wiki ya kwanza ya mwezi Oktoba, 2026. Mvua za Vuli 2026 kwa maeneo hayo zinatarajiwa kuendelea hadi mwezi Januari, 2027.

### Ukanda wa Pwani ya Kaskazini: (kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, mkoa wa Pwani (ikijumuisha kisiwa cha Mafia), Dar es Salaam, Tanga pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):


Mvua za Juu ya Wastani hadi Wastani zinatarajiwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia), kaskazini mwa mkoa wa Morogoro na visiwa vya Unguja na Pemba. Mvua hizo zinatarajiwa kuanza wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Oktoba, 2026 na kuisha mwezi Januari, 2027.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu “N”, Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

### ii. Nyanda za Juu Kaskazini Mashariki: (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):

Mvua za Juu ya Wastani hadi Wastani zinatarajiwa katika maeneo haya. Mvua hizo zinatarajiwa kuanza katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Oktoba, 2026 na kuisha mnamo mwezi Januari, 2027.




***Kielelezo 2: Kushoto: Mwelekeo wa mvua za Vuli (Oktoba –Desemba), 2026 na Kulia: Wastani wa muda mrefu (miaka 30) wa mvua za Vuli (1991-2020).***

***Angalizo 1:*** *Kutokana na uwepo wa El-Niño, vipindi vya mvua vinatarajiwa kwa mwezi Septemba, 2026 katika baadhi ya maeneo nchini. Hata hivyo, mvua za Vuli, 2026 zinatarajiwa kuanza rasmi mwezi Oktoba, 2026 katika maeneo mengi.*

***Angalizo 2:*** *Kuwepo kwa hali ya El Niño kuelekea mwishoni mwa mwaka kunaweza kusababisha kuanza mapema kwa mvua za Novemba 2026 – Aprili 2027 (Msimu) katika baadhi ya maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka, ambako kwa kawaida msimu wa mvua huanza mwezi Novemba.*

***Angalizo 3:*** *Mwelekeo wa mvua uliotolewa hapa umezingatia zaidi kipindi cha msimu (miezi mitatu) na hali ya mvua katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya mvua na mabadiliko ya muda mfupi katika maeneo madogo utazingatiwa katika uchambuzi wa utabiri wa muda wa kati na mfupi. Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia*

*taarifa za utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi na tahadhari kama zinavyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.*

## 2. MIFUMO YA HALI YA HEWA

Katika msimu huu wa Vuli, joto la bahari katika eneo la tropiki ya kati ya Bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuendelea kuwa la Juu ya Wastani, hali inayoashiria uwepo wa El Niño yenye nguvu kubwa. Aidha, joto la bahari la Juu ya Wastani linatarajiwa zaidi katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi ikilinganishwa na eneo la mashariki mwa bahari ya Hindi, hali inayotarajiwa kusababisha upepo wa bahari wenye unyevu kuvuma kuelekea maeneo ya nchi yetu. Vilevile, joto la bahari la Wastani hadi Juu kidogo ya Wastani linatarajiwa katika eneo la mashariki mwa Bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Kwa ujumla, hali hizi za bahari zinatarajiwa kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo mengi ya nchi.

## 3. ATHARI NA USHAURI

Athari za kisekta na ushauri unaotolewa hapa chini umeandaliwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania kwa kushirikiana na wataalam wa sekta husika katika mkutano wa wadau wa hali ya hewa uliofanyika tarehe 14 Agosti, 2026 na semina ya wanahabari iliyofanyika tarehe 17 Agosti, 2026. Wadau wa sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii wanashauriwa kupanga na kutekeleza shughuli zao kwa kuzingatia taarifa mahususi za hali ya hewa zinazotolewa na TMA.

### a) Kilimo na Usalama wa Chakula

Vipindi vya unyevu wa kuzidi kiasi kwenye udongo pamoja na mafuriko vinaweza kujitokeza na kuathiri ukuaji wa mazao na miundombinu ya kilimo. Magonjwa ya mazao yanayosababishwa na kuvu, bakteria na virusi yanaweza kujitokeza. Magonjwa hayo yanaweza kuathiri ukuaji, ubora na mavuno ya mazao mbalimbali, hususan viazi mviringo, alizeti, maharage, ufuta pamoja na matunda na mbogamboga. Mvua za muda mrefu zinaweza kuathiri shughuli za uvunaji na kusababisha upotevu wa mazao baada kuvuna. Hata hivyo, shughuli za kilimo zinatarajiwa kuendelea kama ilivyo kawaida katika baadhi ya maeneo katika msimu huu wa Vuli, 2026.

Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba, kupanda, kupalilia na kutumia pembejeo husika kwa wakati. Pia wakulima wanashauriwa kutumia mbinu bora na teknolojia za kuzuia maji kutuama shambani, mmomonyoko na upotevu wa rutuba; na kuchagua mbegu na mazao sahihi kwa ajili ya msimu huu wa Vuli, kama wanavyoshauriiwa na maafisa ugani na taarifa za hali ya hewa za mara kwa mara. Aidha, inashauriwa kuimarisha miundombinu ya kilimo pamoja na uvunaji maji ya mvua na kudhibiti visumbufu vya mimea. Hatua hizi zitasaidia kupunguza athari za magonjwa na kuongeza uzalishaji

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu “N”, Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe: met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

### b) Mifugo na Uvuvi

Wafugaji na wavuvi wanatarajiwa kunufaika na upatikanaji wa malisho ya mifugo na chakula cha samaki. Hata hivyo, mlipuko wa magonjwa ya mifugo kama vile ugonjwa wa homa ya bonde la ufa, kuoza kwa kwato na kuzaliana kwa wadudu wanaosambaza magojwa vinaweza kujitokeza. Vilevile, matukio ya kuongezeka kwa magonjwa ya mwani baharini na kupungua kwa uzalishaji wa mwani kutokana na kupungua kwa kiwango cha chumvi ya maji ya bahari vinatarajiwa.

Wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji ili kutunza malisho na kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya baadae. Jamii inashauriwa kuweka mipango madhubuti ya matumizi bora ya maji na malisho. Wakulima wa mwani wanashauriwa kulima mwani kwenye maji ya kina kirefu ili kuondokana na athari za maji ya mvua yatakayoingia baharini. Aidha, Wafugaji na wavuvi wanashauriwa kufuatilia mirejeo ya tabiri za hali ya hewa na ushauri kutoka kwa maafisa ugani ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza na kuongeza tija katika msimu huu wa mvua.

### c) Utalii na Wanyamapori

Upatikanaji wa malisho na maji kwa wanyamapori katika mbuga na hifadhi za wanyamapori unatarajiwa kuwa mzuri. Hata hivyo, mvua nyingi zinazotarajiwa zinaweza kusababisha kutuama kwa maji na mafuriko, ambayo yanaweza kusababisha wanyamapori kuhama.

Hali hii inaweza kusababisha hatari ya magonjwa ya wanyamapori kusambaa kwa wanyama wanaofugwa, kutokana na wanyamapori kuingia katika maeneo ya jamii yanayozunguka mbuga na hifadhi za wanyamapori. Hali hiyo inaweza kuongeza uwezekano wa kuongezeka kwa migogoro kati ya binadamu na wanyamapori, na kusababisha hatari kwa binadamu na wanyama wanaofugwa.

Mamlaka husika zinashauriwa kuboresha miundombinu mbalimbali katika hifadhi za wanyamapori na kujenga uelewa kwa jamii ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza kutokana na hali ya mvua inayotarajiwa. Aidha, jamii inashauriwa kutoa taarifa kwa mamlaka husika iwapo wanyamapori wataingia katika makazi au maeneo mbalimbali ya watu ili waweze kudhibitiwa.

### d) Usafiri na Usafirishaji

Matukio ya hali mbaya ya hewa yanaweza kuathiri miundombinu na shughuli za usafirishaji, kwa njia za barabara, reli, bandari na viwanja vya ndege. Athari zinazoweza kujitokeza ni pamoja na mmomonyoko wa udongo, kuporomoka kwa kingo za barabara, uharibifu wa madaraja na njia za reli za MGR na SGR hali inayoweza kupelekea kuongezeka kwa ajali. Aidha, shughuli za upakiaji na upakuaji wa mizigo bandarini zinaweza kuchelewa, hasa kwa shehena zinazohitaji kulindwa dhidi ya unyevu. Kwa ujumla, hali hizi zinaweza kusababisha kuvurugika kwa huduma

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

za usafirishaji, uharibifu wa mizigo na miundombinu, pamoja na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji na matengenezo.
Wadau wa sekta hii wanashauriwa kuchukua hatua stahiki ikiwemo ukaguzi wa mara kwa mara wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

**e) Ujenzi**

Vipindi vya mvua kubwa vinaweza kuathiri sekta ya ujenzi kwa kuchelewesha miradi na kusababisha migogoro ya kimikataba, kuharibu vifaa na miundombinu, kuongeza gharama za ujenzi, kuathiri ubora wa kazi, na kuhatarisha usalama wa wafanyakazi. Pia, mvua nyingi zinaweza kusababisha mmomonyoko wa udongo, uharibifu wa kazi zilizoanza kufanyika na zinazoendelea kutokana na mafuriko kuongezeka kwa unyevu katika majengo, hivyo kupunguza uimara wa miundombinu na kusababisha uharibifu wa vifaa kazi au malighafi.Wadau wanashauriwa kuzingatia utabiri huu wa Vuli katika kuweka sawa mipango ya ujenzi, hasa katika kipindi kinachotarajiwa kuwa na mvua za Juu ya Wastani. Aidha, wanashauriwa kuchukua hatua stahiki pamoja na kuhamisha mitambo mizito na vifaa vya ujenzi kutoka maeneo ya mabonde na chemchemi kabla ya mvua kuanza ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza. Vilevile inashauriwa kununua na kuhifadhi mapema vifaa vinavyoweza kuharibika vikipata unyevu, kama saruji na nondo, katika maghala salama ili kuzuia uhaba na kuepuka kupanda kwa bei wakati wa msimu wa mvua pamoja na kuweka mifumo thabiti ya usalama mahala kazi.

**f) Nishati, Maji na Madini**

Ongezeko la kina cha maji na uchafuzi katika Maziwa, mabwawa na mito linatarajiwa kujitokeza, hali ambayo inaweza kuathiri miundombinu ya rasilimali za maji na nishati. Katika maeneo yenye shughuli za uchimbaji mdogo wa madini, tahadhari stahiki za usalama zinapaswa kuzingatiwa, kwani mvua za Juu ya Wastani zinaweza kuongeza hatari ya maporomoko ya ardhi na kuporomoka kwa mashimo ya uchimbaji yasiyo imara.

Wadau wanahimizwa kuendeleza matumizi endelevu na uhifadhi wa rasilimali za maji katika uchakataji wa madini, uzalishaji wa umeme, shughuli za viwandani, na matumizi ya majumbani. Ingawa mvua za Juu ya Wastani zinatarajiwa kuongeza upatikanaji wa maji, mamlaka husika zinashauriwa kutekeleza hatua stahiki za usimamizi wa rasilimali za maji ili kupunguza hatari ya mafuriko na kupungua kwa ubora wa maji. Aidha, mamlaka husika zinahimizwa kuimarisha ustahimilivu wa miundombinu ya maji na nishati, pamoja na kuendeleza matumizi ya vyanzo mbadala vya nishati, ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza kutokana na mvua kubwa na mafuriko yanayotarajiwa.

**g) Mamlaka za Serikali za Mitaa**

Vipindi vya mvua kubwa vinaweza kusababisha kutuama kwa maji na mafuriko. Hali hii inaweza kusababisha uharibifu wa miundombinu na upotevu wa maisha na mali. Mamlaka

za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuboresha mifumo ya mifereji ya maji ili kupunguza athari zinazoweza kusababishwa na mafuriko sambamba na kutoa elimu kwa jamii juu ya hatua zinazopaswa kuchukuliwa. Hatua hizo ni pamoja na kuimarisha kamati za maafa katika ngazi za vijiji na wilaya ili waweze kujiandaa, kukabiliana na kupunguza athari pindi zitakapotokea.

### h) Sekta ya Afya

Magonjwa ya mlipuko yanaweza kujitokeza kutokana na uharibifu wa miundombinu ya maji taka unaoweza kusababishwa na maji kutuama na kutiririka. Mamlaka zinazohusika na afya pamoja na jamii zinashauriwa kuchukua hatua stahiki za kiafya ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza. Hatua hizo ni pamoja na kutokomeza mazalia ya mbu, kuhakikisha upatikanaji wa akiba ya kutosha ya dawa na vifaa tiba, pamoja na kujiandaa kwa changamoto zinazoweza kujitokeza kutokana na uharibifu wa miundombinu ya usafiri. Vituo vya afya vinashauriwa kuwa na mipango mbadala ya kuhakikisha mwendelezo wa huduma za afya.

### i) Sekta Binafsi

Sekta binafsi inatarajiwa kunufaika na mvua za kutosha zinazotarajiwa katika msimu huu wa Vuli ikiwa ni pamoja na baadhi ya shughuli za kilimo, uzalishaji viwandani, n.k. Hata hivyo, kutokana na wingi wa mvua za Juu ya Wastani hadi Wastani, unaweza kusababisha athari katika shughuli za kijamii na kiuchumi zikiwemo ujenzi na miundombinu, kilimo, uhifadhi na usafirishaji wa mazao na bidhaa.

Wadau wa Sekta binafsi wanashauriwa kushirikiana na wataalamu mbalimbali ikiwemo wataalam kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa ili kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza. Taasisi za Benki na Bima zinashauriwa kuandaa na kutoa huduma mahususi kwa wadau ili kujenga ustahimilivu katika biashara.

### j) Menejimenti za Maafa

Vipindi vya mvua kubwa vinatarajiwa kujitokeza na kusababisha mafuriko na maporomoko ya ardhi katika baadhi ya maeneo. Hali hii inaweza kupelekea madhara kwa binadamu, wanyama na mazingira, uharibifu wa miundombinu, kuathiri utoaji wa huduma za kijamii, kiuchumi na upotevu wa mali. Hivyo, Idara ya Menejimenti ya Maafa nchini inashauriwa kuendelea kuratibu utekelezaji wa mipango itakayosaidia kupunguza madhara yanayoweza kujitokeza. Aidha, Sekta, Mamlaka husika, na Kamati za Usimamizi wa Maafa katika ngazi za Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji/Mitaa zinashauriwa kushirikiana na kuchukua hatua stahiki, ikiwa ni pamoja na kutoa tahadhari za mapema, kutoa elimu na miongozo itakayowezesha kuzuia au kupunguza madhara, kujiandaa, kukabiliana na maafa, na kurejesha hali endapo maafa yatatokea.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**k) Vyombo vya Habari**

Waandishi wa habari wanashauriwa kupata na kusambaza utabiri na tahadhari rasmi za hali ya hewa zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) pekee, ili kuhakikisha taarifa sahihi zinawafikia wananchi kwa wakati kwa ajili ya kuongeza uelewa na kuimarisha maandalizi dhidi ya athari zinazoweza kusababishwa na hali mbaya ya hewa. Kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Na. 2 ya Mwaka 2019, ni kosa kisheria kusambaza taarifa za hali ya hewa kutoka katika vyanzo visivyo rasmi.

Aidha, waandishi wa habari wanashauriwa kutafuta mwongozo wa kitaalamu unaohusu sekta na wataalam husika na kuwasilisha taarifa za hali ya hewa kwa lugha iliyo wazi na rahisi, ili kuongeza uelewa wa umma na kusaidia maandalizi madhubuti dhidi ya athari za hali mbaya ya hewa.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wote wa taarifa hii ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, mamlaka za wanyamapori, usafiri na usafirishaji, mamlaka za maji, na afya kuendelea kutafuta, kupata na kuzingatia ushauri wa wataalam katika sekta husika.*

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania itaendelea kufuatilia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na kutoa mirejesho ya mwelekeo wa mvua nchini kadri inavyohitajika. Aidha, wadau wanashauriwa kuwasiliana na Mamlaka ili kupata taarifa mahsusi za utabiri wa msimu ili kukidhi mahitaji maalum katika sekta zao.*

***Imetolewa: 18 Agosti, 2026***

**Na: Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**